

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam
Tarehe 30 June 2007**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishekh
Elaine Baker
Emmy Rashidy
Faraji Kiruwa
Ima Mhigai
Juma Hassani Mibweto
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Mrisho Salumu Lumuli
Ramadhani Rajabu Nyengo
Rashidi Saidi Karanji
Shabani Ramadhani
Sudi Saidi

Wanachama wapya

Walikuwepo wanachama wageni wanne na Emmy kama mmoja wa wanawake alipewa ukaribisho wa pekee. Tulijadili umuhimu wa kuwapata wanawake zaidi.

Akaunti ya Benki

Elaine aliarifu kuwa alipiga simu National Microfinance Bank (NMB). Orodha ya vitu vinavyohitajika ni kama ifuatavyo:

- Tsh 11,000 ya kufungua akaunti
- Barua kutoka serikali za mitaa/kata ikitambulisha kikundi na sahihi.
- Picha ndogo (stampsized) za kila aliyetia sahihi zilizopigwa mhuri wa serikali za mitaa.
- Cheti cha usajili ch kikundi.
- Barua ya UWABA ya kuomba kufungua akaunti kwa meneja wa benki.
- Mapendekezo toka kwa wateja hai wa benki ya NMB
- Nakala ya katiba ya UWABA
- Sahihi zote zinatakiwa benki ili kufungua akaunti.

Ingawa barua yetu ya utambuzi ilitoka serikali za mitaa mwenge, ilionekana kuwa ni vyema tukipata nyingine kutoka Mahakama ya ndizi kwa sababu tunataka kufungua ofisi huko.

Ally Saidi Mohammed atafuatilia mawasiliano na serikali za mitaa Mahakama ya Ndizi kupata barua. Atajaribu pia kupata wateja wa NMB. Elaine alisema atapata picha tatu za wenye ofisi itakuwa rahisi kutengeneza nyaraka nyingine.

Ofisi

Jumanne aliarifu kuwa ofisi tutakayopata ni yenye geti jekundu. mwenye nyumba anataka Tsh 20,000 kwa mwezi na kodi iwe kwa miezi 12. Alisema kuwa hajapata majibu kwa watu aliowaomba wachangie UWABA. Iliamuliwa kwamba wanachama watachangia Tsh 5,000 kama wataweza, kwa kiwango kidogo kidogo kili wiki, na Elaine atatafuta vyanzo vingine vya fedha ikiwemo ITDP.

Ilikubalika kuwa tutapaka rangi kuta za ofisi, tutatundika ubao wa matangazo na rafu ya vitabu ili kuweka nyaraka na taarifa kiti na meza na baadhi ya benchi.

Msafara wa Baiskeli

Juma alimwambia Elaine kuwa alifanikisha kusambaza barua zilizosalia Bakhresa na kwamba alifanikiwa kuongea na Bakhresa mwenyewe. Bwana Bakhresa alitaka kujua kama tuna akaunti ya Benki. Zantel ilikataa kuwa wafadhili kwa madai kwamba haiendani na orodha yao ya fedha. Iliamuliwa kufuatilia Celtel.

Elaine alikosa muda wa kufuatilia kwa simu wiki iliyopita lakini aliahidi kufuatilia wiki itakayofuata na kujaribu kupanga mikutano.

Barabara zilizo katika mpango wa ujenzi

Mmoja wa washauri wa kampuni, Carl Bro Associates ambaye ni mshauri wa Barabara ya Nelson Mandela alijibu UWABA kwa barua pepe, akashauri kwamba ni bora kuwasiliana na TANROADS moja kwa moja kwani wao wameshamaliza tangu mwezi Februari Elaine aliwauliza ikiwa tutaweza kuwapigia simu kuwauliza maswali nao wakakubali. Elaine atapiga simu wiki hii kupanga mkutano na kuwaarifu wengine.

Mpango madhubuti wa usafiri Dar es Salaam

Elaine alisoma kwenye gazeti kuwa serikali inashirikiana na kampuni ya Japani International Cooperation Agency (JICA) ili kuandaa mpango madhubuti wa usafiri Dar es Salaam pia wanachama walishuhudia baadhi ya watu wakikusanya maelezo kuhusu idadi ya magari yanayopita penye makutano wiki hii. Elaine aliuliza kundi mojawapo na kiongozi wao alimjibu kuwa wao ni wanafunzi wa chuo cha usafirishaji Dar es Salaam na walikuwa wanakusanya maelezo kwa ajili ya kuandaa mpango huo. Alisema kuwa mtu wa kuwasiliana nae chuoni hapo ni Bwana Wemba. Elaine aliandaa barua kwa Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, JICA na Taasisi ya usafirishaji kuomba UWABA wawekwe kama wadau katika mpango huo.

Mengineyo

Elaine alisambaza utambulisho kwa wanachama na walitakiwa kuchangia Tsh 500 na Jumne alihifadhi orodha kwa niaba ya Juma. Lijadiliwa kuwa UWABA wawe T – shirt na kila mwanachama anunue naziwe na kauli mbiu ya UWABA.